

# UTUKUFU WA MUNGU

Marcus Mtinga
22.10.2005 Tabata DSM






2.Furahi sana binti Sayuni piga makofi, Mwenyezi Mungu amesikia kilio chako,
Amewatupa chini wenye enzi na viti vyao, amewakweza wanyonge rehema zake zikawa kwako,
Kweli Mwenyezi Mungu..........

3. Tumeuona wema wako mwenyezi Mungu, upole wako unatupunguzia uchungu,
katika maisha yetu unatufunza kuvumilia, magumu yakitusonga watupa moyo tunayabeba,
Kweli Mwenyezi Mungu.........

4. Matatizo yetu unayajua vema Baba, udhaifu wetu unaujua vema sana tu!
Sisi peke yetu Baba hatutaweza kufika vema, msaada wako mwema huruma yako utupe hima
Kweli Mwenyezi Mungu..........

5. Tunayakabidhi maisha yetu moyoni mwako, furaha, dhiki taabu zetu viwe ni vyako,
Utulinde ututunze kwa nguvu zako tuwe salama, na hii safari yetu kurudi kwako iwe salama,
Kweli Mwenyezi Mungu....